JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHURI YA MJI NJOMBE.

SHULE YA SEKONDARI MATOLA,
S.L.P 169,
NJOMBE.
25.04.2024

BARUA PEPE: matolasecondary@gmail.com.
NAMBA YA SIMU: 0755684800/0685729712.
Kumb. Na MTSS/J.1/VOL.II/32.

JINA LA MWANAFUNZI..............................................................
S.L.P................................................
............................................................

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA MATOLA KWA MWAKA WA MASOMO 2024/2025

## 1.0 UTANGULIZI.

Nina furahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari ya MATOLA mwaka wa masomo 2024/2025. Shule hii ipo katika Mkoa wa Njombe, Halmashauri ya Mji Njombe.Ipo umbali wa **kilometa 65** Kusini mwa Mji wa Njombe, Usafiri wa basi kutoka mjini NJOMBE unapatikana katika kituo cha mabasi cha NJOMBE, nauli ni **TSHS 5,000/=.**

**Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 01/07/2024. Hivyo unatakiwa kuripoti shuleni Tarehe 30/06/2024. Mwisho wa kuripoti ni Tarehe 07/07/2024. Baada ya hapo nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine**

Karibu Sana Matola Sekondari,

Wako,

GIDEON D. MASSAO
MKUU WA SHULE
0755 684 800/0687335954

MKUU WA SHULE
MATOLA SEKONDARI
S.L.P. 169
NJOMBE

## 2.0. MICHANGO YA SHULE

Kuna michango mbalimbali ambayo kila mwanafunzi anatakiwa kuilipa mara anaporipoti shuleni. Michango hiyo ni kama ilivyoainishwa hapa chini;

| | | |
|---|---|---|
| i. | Michango ya uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| ii. | Kitambulisho | 5,000/= |
| iii. | Nembo ya Shule | 5,000/= |
| iv. | Tahadhari | 5,000/=(haitarudishwa) |

NB. Mwanafunzi asiye na kadi ya bima ya afya aje Tsh 30,000/= kwa ajili ya bima ya afya iliyoboreshwa. FEDHA HII ISILIPWE BENKI. Kama ana bima ya afya aje nayo.

**JUMLA YA MICHANGO YOTE = 80,000/=**

**NB: MICHANGO YOTE ILIYOAINISHWA HAPO JUU ILIPWE BANK KUPITIA AKAUNTI NAMBA 60610003731 NMB. USIJE NA PESA TASLIM SHULENI ISIPOKUWA TSH 30,000/= KWA AJILI YA BIMA YA AFYA.**

### 2.1 SARE ZA SHULE.

(a) Sare ya shule hii ni:

a. DARASANI.

- Mashati mawili meupe (Tetroni) mikono mirefu.
- ***Suruali mbili rangi ya daki bluu ziwe na turn up na upana chini uwe 18cm.***
- Soksi rangi nyeusi jozi Tatu.
- Sweta mbili rangi ya kijivu (grey) ziwe za **KUFUMWA SIO MKENYA AU INDIA.** Kama kwenye mazingira unayotoka hazipo,Zinapatikana katika maduka yaliyo jirani na shule kwa shilingi 13,000/=
- Mkanda mweusi(wa ngozi),
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba vyenye visigino vifupi pea mbili kwa ajili ya darasani.
- ***Suruali nyeusi kwa ajili ya kazi za nje iwe na turn up pia upana chini uwe 18cm.***
- Pull neck rangi nyeupe.
- ***Tai mbili za rangi ya dark bluu.***
- T-shirt ya kijivu yenye kola(iwe ya cotton) Kama kwenye mazingira unayotoka hazipo,zinapatikana kwenye maduka yaliyo jirani na shuleni kwa Tsh 12,000/=
- Laboratory coat rangi nyeupe (Aje nalo)
- Dissection kit seti moja (Aje nayo)
- ***SAA YA MKONONI KWA MATUMIZI YAKE NI LAZIMA KWA SABABU SHULENI HAKUNA MATUMIZI YA KENGELE.***

(b)MICHEZO.

- Viatu vya michezo aina yoyote
- **Track suit Nyeusi ya mtelezo yenye mistari myeupe pembeni**
- Jezi rangi ya njano (tshirt na bukta).
- Nguo za ndani kuanzia tano (5) na kuendelea.

2.2 VIFAA VINGINE VYA DARASANI.

- Daftari *counter Books 12 quire 3.*
- Mkebe wenye Vifaa vya Hisabati, kalamu ya risasi (Penseli), kalamu za wino za kutosha.
- Kamusi ya kingereza kwa kingereza moja (Dictionary – English to English) ni muhimu.
- Bunda (rimu) mbili za karatasi A4 **(LILILOANDIKWA (NO.1 MONDI)**
- Faili gumu kwaajili ya kuhifadhia karatasi zako za mazoezi na majaribio mbalimbali.
- Scientific calculator (fx 991)
- Graph paper pad zisipungue 05 kwa ajili ya matumizi yako.
- **AJE NA VITABU ambavyo vimeoneshwa kwenye kiambata**

**1.3 . MAHITAJI YA BWENINI.**

a) Godoro moja la futi $2\frac{1}{2}$ ( mbili na nusu) inchi 3, uje nalo.
b) Blanketi moja.
c) Shuka mbili rangi ya pink.
d) Ndoo mbili za plastiki lita kumi kwa matumizi yako binafsi.
e) Vyombo vya kulia chakula yaani, sahani, bakuli, kijiko na kikombe.
**f)** Sanduku madhubuti kwa ajili ya kuhifadhia mahitaji yako.
**g)** Taulo moja
**h)** Mto
i) shoka lenye mpini wa mti
j) Chelewa 01, hard broom 01, drier 01 na soft broom 01

TANBIHI:

1. Kila mwanafunzi awe mlinzi wa mwenzake kuzuia uovu unaoweza kujitokeza katika chumba chao. Uharibifu wowote ule ukitokea/ ukibainika katika chumba kimoja wapo wanafunzi wanaoishi katika chumba hicho wataadhibiwa kwa sababu wote watakuwa wameshiriki katika uharibifu huo.
2. Uharibifu wowote utakaosababishwa na mwanafunzi ni jukumu la mwanafunzi husika na mlezi/ mzazi wake.
3. ***Kamwe nguo za nyumbani haziruhusiwi hapa shuleni hivyo usije nazo.***
4. ***Mwanafunzi Haruhusiwi kuingia shuleni na vyakula vilivyopikwa au vibichi kutoka nyumbani au mahali pengine popote.***

*5. Mwanafunzi akitoroka shule atatakiwa kulipa waya wa uzio wenye urefu wa mita 15 na upana wa mita 2.5 au trip moja ya mawe kwaajili ya ujenzi wa uzio*

## MASHARTI MENGINE.

1. MAWASILIANO TOKA KWA MZAZI /MLEZI
   - Maagizo yote ya fedha au mizigo vitumwe posta tu, ambapo mhudumu wa shule anaweza kuchukua na kuleta shuleni. Aidha taarifa nyingine inayomhusu mwanafunzi mfano kufiwa itumwe kwa Mkuu wa Shule na si kupitia mwa mwanafunzi

2. USAFI BINAFSI PAMOJA NA MAZINGIRA.
   - Unatakiwa kuja Shuleni na nywele fupi, usinyoe panki au upara, hairuhusiwi kufuga ndevu wala kucha. Aidha unatakiwa kuwa msafi na uoge mara kwa mara, sambamba na haya unatakiwa kuyatunza mazingira ya Shule katika hali ya Ubora na safi siku zote.
3. USHIRIKI KATIKA KAZI ZA MIKONO
   - Ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki katika kazi za mikono ambazo zina lengo la kuendeleza Elimu ya Kujitegemea pamoja na Kuimarisha afya ya mwili.
4. NIDHAMU.
   - Ili uweze kujifunza na kufaulu katika masomo yako unatakiwa kuwa na Nidhamu ya hali ya juu, unatakiwa kuzisoma na kuzielewa sheria za Shule zilizoambatanishwa na fomu hii. Pia ifahamike kuwa si jukumu la shule kutoa Nauli kwa mwanafunzi pindi anapopatikana na makosa ya kinidhamu ya kumrudisha nyumbani, ni wajibu wa mzazi /mlezi wa mwanafunzi.
5. MICHEZO NA UTAMADUNI
   - Unatakiwa kushiriki Michezo na Utamaduni kwa lengo la kuleta uhusiano mwema na kujenga miili yenye afya. Aidha jitokeze na ibua kipaji chako katika fani mbalimbali mfano kuimba, kuigiza, skauti na kadhalika.
6. DINI.
   - Kila mwanafunzi anaruhusiwa kufanya ibada kulingana na Imani yake ili mradi shughuli hizo zitaendeshwa kwa kufuata sheria na kanuni za Nchi pamoja na Ratiba ya Shule. Aidha mwanafunzi ataswali/Sali shuleni au maeneo yaliyo karibu na shule tu.
7. **CHAKULA MAALUMU.**
   - Shule haitatoa chakula maalumu kwa wanafunzi tofauti na wengine, Aidha mzazi / mlezi unashauriwa umtafutie mahali ambapo ataweza kusoma na kupata huduma ya chakula kulingana na tatizo la mwanafunzi.

## 3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na teknolojia, yenye dhamana ya Elimu nchini na OFISI YA RAIS - TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Mashutumu,matusi na kupigana ni marufuku.
2. Mwanafunzi ni lazima awe mtii na mwenye heshima kwa mkuu wa shule, walimu, watumishi wasio walimu na watu wote kwa ujumla wakati na mahali popote ndani na nje ya shule.
3. Mwanafunzi atatakiwa kuhudhuria vipindi vyote darasani,nje ya darasa na kazi zote za mikono kwa muda wote wa masomo yake.
4. Mwanafunzi atasimama (ikiwa alikaa) na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote.
5. **Mwanafunzi anatakiwa kuongea lugha ya kiingereza wakati wote awapo shuleni**.
6. Nimarufuku mwanafunzi kuvuta sigara, bangi, kunywa pombe, madawa ya kulevya , kuleta vileo shuleni au kuonekana mahali penye ulevi wakati wote wa masomo.
7. Wizi wa aina yoyote ni kosa kubwa, adhabu ni kufukuzwa shule na kupelekwa mahakamani.
8. Nimarufuku mwanafunzi yeyote kujihusisha na uasherati awapo mahali popote kwa muda wake wa masomo.
9. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea maeneo ya ofisi ya mkuu wa shule, ofisi ya walimu,nyumba za walimu na wafanyakazi ila kwa kibali maalumu.
10. Nimarufuku mwanafunzi kuoa au kuolewa, kupata au kusababisha mimba au kutoa mimba.
11. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule awapo darasani,kwenda hospitali, maandamano halali, kusafiri kuja na kurudi nyumbani na mahali popote atakapo ruhusiwa.
12. **Mwanafunzi haruhusiwi kupaka manukato, kupaka rangi za mdomo na kucha, kuvaa kofia, viatu vya ghorofa, kidani, mkanda mpana, kuvaa hereni, pete, mkufu awapo shuleni.**
13. Mwanafunzi haruhusiwi kufuga ndevu, kuwa na kucha ndefu, nywele ndefu. Hairuhusiwi kunyoa nywele mtindo wa denge/punk. Wasichana hawaruhusiwi kusuka nywele mtindo wowote
14. Vifaa vyote vya shule ni mali ya umma mwanafunzi hana budi kuvitunza kwa uangalifu. Uharibifu wa makusudi wa aina yoyote ni marufuku na lazima kulipia uhalibifu unao tokea.
15. Upigaji kelele na soga mahali popote penye mkusanyiko rasmi darasani, mistarini, “parade” nk. Ni marufuku.
16. Nimarufuku mwanafunzi kuendesha shughuli za vyama vya siasa shuleni. Vilevile mwanafuzi haruhusiwi **kuvaa mavazi yanayotumiwa na chama chochote cha siasa**.
17. Mwanafunzi anayefikiwa na mgeni ni budi amtaarifu mwalimu wa zamu.

18. **Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki/kuwa na simu, chaja ya simu, laini za simu na vifaa vingine vyovyote vinavyohusiana na simu muda wote awapo shuleni. Akikutwa navyo atanyang'anywa na kufukuzwa shule.**

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA/ KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi
b) *Utoro*
c) Uasherati na ushoga
d) Ubakaji na ulawiti
e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine,mirungi, kubeli na kadhalika.
f) Kupigana au kupiga.
g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
h) Kudharau Bendera na wimbo wa Taifa.
i) Kuwa mjamizito/ kupata mimba.
j) Kuoa au kuolewa.
k) Kutoa mimba.
l) Kugoma, kuchochea na kuongeza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
m) Kukataa adhabu kwa makusudi.
n) **KUMILIKI KIFAA CHOCHOTE CHA SIMU. HIVYO NI MARUFUKU KUJA NA SIMU SHULENI.**

**3.2. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA WANAFUNZI.**

a) Medical Examination fomu ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

***"TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO / MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU".KAMA HUJAELEWA SEHEMU YOYOTE TAFADHALI PIGA SIMU NAMBA 0755684800 AU 0685729712***

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja MATOLA SEKONDARI

KARIBU SANA

...........................

MKUU WA SHULE
GIDEON D. MASSAO

NAKALA KWA:

1. Katibu ,
   Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,
   S. L. P 1923,
   DODOMA.
2. Katibu Tawala Mkoa,
   S. L. P 668,
   NJOMBE.

3. Mkurugenzi,
   Halmashauri ya Mji Njombe,
   S. L. P 577,
   NJOMBE.

OFISI YA RAIS (OR) TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE
SHULE YA SEKONDARI MATOLA

FOMU YA KUKUBALI NAFASI

1. MWANAFUNZI.

Jina la mwanafunzi…………………………………………………………………………
Anuani
………………………………………………………………………………………..

**Nimekubali/Sijakubali kujiunga na jumuiya ya Shule ya Sekondari ya Matola.**
**Nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa. Ninaahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria na taratibu za shule kama Nitakavyoelekezwa.**

Sahihi ya mwanafunzi …………………………………………..
Tarehe …………………………………….

2. <u>MZAZI/MLEZI</u>

Mimi ………………………………………………………………………………………………
Mzazi/Mlezi wa ………………………………………………………………………………
Nimesoma kwa makini maagizo yaliyotolewa yanayohusu mtoto wangu.
Nimekubali/Sijakubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo.

Naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu **kielimu** na **kimalezi.**

Sahihi ya mzazi/mlezi ………………………………………
Namba ya simu……………………………………………
Tarehe ……………………………………

**OFISI YA RAIS (OR) TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA MJI NJOMBE**
**SHULE YA SEKONDARI MATOLA.**

MAELEZO BINAFSI:-

1. Jina lako ……………………………………………. Kidato cha ………………….. Tarehe ya kuzaliwa ………………………. Mahali ulipozaliwa ………………………………… Wilaya…………. Dhehebu …………….. Shule ya msingi ulikotoka …………………
2. **<u>BABA</u>**
   a) Jina la baba……………………………………..
   b) Yu hai/amefariki ………………………………………………
   c) Anuani yake kama yu hai …………………………………………..
   d) Kazi yake ……………………………………………………….
   e) Ameajiriwa na idara gani?..........................................
   f) Dini ya baba ni …………………………………………………
   g) Namba ya simu ……………………………………………………..

3. **<u>MAMA</u>**

a) Jina la mama……………………………………..
b) Yu hai/amefariki ………………………………………………
c) Anuani yake kama yu hai …………………………………………..
d) Kazi yake ……………………………………………………….
e) Ameajiriwa na idara gani?..........................................
**f)** Dini ya mama ni …………………………………………………
g) Namba ya simu ……………………………………………………..

4. **<u>MLEZI</u>**

Unaye mlezi, Mlezi ni mtu yeyote ambaye si mzazi wako lakini anakutunza na kukulipia gharama zote na mahitaji yako) NDIO/HAPANA.

Kama jibu ni ndio:-

a) Jina la Mlezi ……………………………………………………..
b) Uhusiano na mlezi (Mjomba,Shangazi,kaka n.k)……………………………………
c) Anuani yake ……………………………………..
d) Dini ya mlezi ………………………………………
e) Kazi yake …………………………………………
f) Ameajiliwa na idara gani? ………………………………………
g) Namba ya simu ……………………………………………………..

5. ANUANI YA BABA AU MAMA AU MLEZI ATAKAYEKUWA ANAWASILIANA NA SHULE.
   ………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………
   NAMBA YA SIMU ……………………………………………………………
   JINA NA SAHIHI YAKE ………………………………………………………

6. MAJINA YA NDUGU WENGINE WANAOHUSIKA NA MALEZI YA MWANAFUNZI HUYU
   1. Ndugu ………………………………………………………………
      Anuani yake……………………………………………………………
      Namba ya simu………………………………………………………..

   2. Ndugu ………………………………………………………………
      Anuani yake…………………………………………………………..
      Namba ya simu………………………………………………………

7. ANUANI YA OFISI YA KATIBU KATA/MWENYEKITI WA MTAA/KIJIJI ANAKOISHI MZAZI/ MLEZI

   1. Jina la Katibu Kata…………………………………………………………
      Kata ya…………………………………………………………………………
      Anuani …………………………………………………………………………
      Namba ya simu…………………………………………………………...

   2. Jina la Mwenyekiti wa mtaa/Kijiji…………………………………………………………
      Mtaa / Kijiji cha…………………………………………………………
      Anuani …………………………………………………………………..
      Namba ya simu……………………………………………………..

PRESIDENT'S OFFICE – RALG
NJOMBE TOWN COUNCIL
MATOLA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 169
NJOMBE.

## MEDICAL CERTIFICATE FORM.

To be completed by the medical officer in respect of form on entrants.
Pupil's full name ……………………………………………………………………….
Age ………………………….year …………………… sex……………………………………
Blood Count ( Red and White) ……………………………………………………….
Stool Examination …………………………………………………..
Urine Analysis ……………………………………………………………………………
Syphilis
……………………………………………………………………………………………
T.B Test ……………………………………………………………………………………
Eye ………………………………………………………………………………
Ears ………………………………………………………………………………………
Chest
…………………………………………………………………………………………….
Spleen
……………………………………………………………………………………………
Abdomen
……………………………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION** e.g Physical defects or impairments chronic or family diseases.
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
I certify that the above is fit/unfit for admission into day/boarding school.
Signature ………………………………………………………………
Designation ………………………………………………………………..
Station ……………………………………………………………………………..

Date ………………………………… Stamp …………………………………….

## *LIST OF BOOKS PER SUBJECT.*

A. CHEMISTRY
   a. Advanced Chemistry Review by William W. Davis (Mzumbe book shop project,2004)
   b. Physical Chemistry by Delungu e t(Mzumbe book shop project 1998)
   c. Advanced Level Inorganic Chemistry part I and II (Tanzania Institute of Education 1995)
   d. Organic Chemistry Volume I, The Fundamental Principles by I.L Finar (Longman Ltd 1990)

B. BIOLOGY
   a. New Understanding Biology By Suzan Toole
   b. Advanced Biology Principles and Application by C.J. Clegg and D.G Mackean
   c. Advanced Biology by Michael Kent

C. GEOGRAPHY
   a. Principle of Physical Geography by F.J Monkhouse
   b. Geography: Integrated Approach by D. Waugh
   c. Practical Geography for Africa by J.M Pritchard
   d. Simplified Physical Geography (A-Level) by D. M Mapunda
   e. General Geography in Diagram by R.B Bunnert
   f. Statistical methods and the Geographer by S. Gregory
   g. Certificate Physical and Human Geography by Goh Chang Leong